# DISTINCTION NATIONAL EXAMINATION PANEL

007

007

## DARASA LA SABA

## JARIBIO LA SABA - 2021

7

ROYAL

**Muda: Saa 1 Dak 40**

# KISWAHILI LUGHA

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.

2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.

3. Ukisha chagua jibu lolote lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.

5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu zako wewe mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.

7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.

8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.

9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ni sahihi. Chagua jibu hilo.

10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    *Mfano*

    **21.** Kamilisha methali: Ukiona vyaelea________

    A. vyaenda    B. vyaundwa
    C. vyazima    D. vyaisha

    Jibu sahihi ni B

    **Katika karatasi ya majibu**

    **11** [A] [B] [C] [D]    **21** [A] ~~[B]~~ [C] [D]    **31** [A] [B] [C] [D]    **41** [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilochochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku

12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Karatasi hii ya maswali ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

007

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Majuto alikata ___1___ kuacha masomo na ___2___ mjini. Moyoni ___3___ kuwa maisha yangekuwa rahisi kwa sababu wenzake walikuwa wamemdanganya hivyo. Alijua kuwa ___4___ na walimu kuwa afanye kazi za ziada ama kazi za darasani. Aliwasili mjini mwendo wa ___5___, jua lilikuwa likielekea kuzama. Mkononi ___6___ palikuwa na mkoba uliokuwa na nguo zake. Ajabu ni kwamba pindi aliposhuka kutoka ___7___ matatu alimosafiria, alizabwa kofi hadi akaona vimulimuli. Kufumba na kufumbua, alijipata akiwa ameanguka matopeni ___8___! Hakujua mkoba wake ulikoelekea wala la kufanya. Keshoye asubuhi, alianza harakati za kurudi nyumbani kwao.

**1.** A. kauli B. shauri C. kamba D. tamaa

**2.** A. kukimbilia B. kukimbia C. kukimbizwa D. kukimbiza

**3.** A. aliwaambia B. alikuambia C. aliniambia D. alijiambia

**4.** A. hangesumbuliwa B. asingesumbuka C. asingesumbuliwa D. hangesumbuka

**5.** A. machweo B. adhuhuri C. alfajiri D. macheo

**6.** A. kwake B. mwake C. wake D. pake

**7.** A. kwa B. katika C. ndani mwa D. mwenye

**8.** A. chubwi B. pu C. tapwi D. tumbwi

Michezo yoyote ___9___ huwa na manufaa maishani. Mtu ambaye ___10___ michezoni huimarisha afya yake. ___11___ rahisi kwa mtu kama huyo kupatwa na ___12___ ambazo huwapata wengine kwa urahisi. Ikiwa hutaki ___13___ mara kwa mara, ni vyema ujitolee kufanya mazoezi au kucheza kila wakati. ___14___, michezo hujenga umoja na ushirikiano. Wanamichezo lazima washirikiane ili kupata ushindi. Katika hali hii, kila mchezaji huelewa kuwa ___15___.

**9.** A. yale B. zile C. ule D. ile

**10.** A. anayeshiriki B. hushiriki C. ashirikiye D. mwenye hushiriki

**11.** A. Si B. Ni C. Huwa D. Hua

**12.** A. magonjwa B. ndwele C. ugonjwa D. maradhi

**13.** A. kugonjeka B. kuungua C. kuunguzwa D. kuugua

**14.** A. Maadamu B. Ama C. Wala D. Aidha

**15.** A. mgaagaa na upwa hali wali mkavu B. panya wengi hawachimbi shimo
C. kidole kimoja hakivunji chawa D. mchezo kwao hutuzwa

***Kuanzia swali la 16 hadi 30, lijibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua nomino iliyoundwa kutokana na kitenzi.
- A. cheza – mchezo
- B. masomo – soma
- C. vumilia – mvumilivu
- D. mcheshi – cheka

**17.** Methali gani yenye maana sawa na '**mtoto umleavyo ndivyo akuavyo**'.
- A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
- B. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
- C. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi.
- D. Mwana hutazama kisogo cha nina.

**18.** Chagua sentensi iliyoakifishwa kwa usahihi.
- A. Musa alipewa zawadi nyingi; vitabu, kalamu, madaftari, vifutio na kadhalika.
- B. Mimi sipendi mchezo wako, "mama alimwambia Bakari."
- C. Bwana Mwinyi Masharubu (mwalimu wetu wa Kiswahili) amenunua gari.
- D. Ugonjwa wa UKIMWI ni hatari: hauna tiba

**19.** Tambua wingi wa, '**Mtume alipikiwa mkunga akala kwa ugali.**'
- A. Watume walipikiwa wakunga wakala kwa ugali.
- B. Watume walipikiwa mikunga wakala kwa ugali.
- C. Mitume walipikiwa wakunga wakala kwa ugali.
- D. Mitume walipikiwa mikunga wakala kwa ugali.

**20.** Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mistari.

Chakula kitamu kimepikwa vizuri.
- A. kivumishi, kielezi
- B. kivumishi, kivumishi
- C. kielezi, kielezi
- D. kielezi, kivumishi

**21.** Chagua kiunganishi kilicholinganishwa na maana yake kwa usahihi.
- A. angalau – mara nyingi
- B. madhali – kwa mfano
- C. minghairi ya – pasipo
- D. sembuse – fauka ya

**22.** Sentensi ifuatayo itaandikwaje katika ukubwa?

**Uso wa mbuzi uliumizwa na ndovu.**
- A. Kijuso cha kibuzi kiliumizwa na kidovu.
- B. Juso la buzi liliumizwa na dovu.
- C. Jiuso wa jibuzi uliumizwa na jidovu.
- D. Juso la jibuzi liliumizwa na jidovu.

**23.** Numbi ni kwa 'samaki' kama vile ________ ni kwa maua.
- A. korija
- B. bumba
- C. darzeni
- D. koja

**24.** Sentensi gani iliyotumia 'karibu' kuonyesha **nusura**?
- A. Darasa letu limejengwa karibu na afisi.
- B. Mvua karibu ianze kunyesha.
- C. Karibu nyumbani mgeni wetu.
- D. Paka yule karibu aangukiwe na mti.

**25.** Mtu anayeleta na kupeleka barua posta huitwa ________
- A. tarishi
- B. mshenga
- C. mtumwa
- D. mhazili

**26.** Orodha gani yenye nomino za **ngeli ya KI – VI** pekee?
- A. chamcha, chupa, chawa
- B. kengele, kalamu, karai
- C. kiziwi, kipofu, kipepeo
- D. Kiswahili, cherehani, kijibwa

**27.** Mtu anayehamia katika nchi isiyokuwa yake na kuishi huko huitwaje?
A. mzalendo
B. mlowezi
C. mwenyeji
D. kibaraka

**28.** Tambua sentensi ambayo **ni sahihi**.
A. Wachezaji wote wamewasili uwanjani.
B. Wachezaji wote wamewasili katika uwanjani.
C. Wachezaji wote wamewasili ndani ya uwanjani.
D. Wachezaji wote wamewasili uwanja.

**29.** Neno gani lenye silabi tano kati ya maneno yafuatayo?
A. ambia
B. cheza
C. tumbukia
D. tekelezea

**30.** 'Mama alipika chakula cha mtoto.' Ndiko kusema kuwa;
A. Mtoto alipikwa chakula na mama.
B. Chakula cha mtoto kilipikwa na mama.
C. Mama alimpikisha mtoto chakula.
D. Mama alipikiwa chakula na mtoto.

***<u>Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 31 - 40</u>.***

Maendeleo ya nchi hutegemea mchango na juhudi za kila mwananchi. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha kuona kuwa baadhi yetu tuna fikira zisizo za kizalendo kuwa wengine ndio wanaopasa kuiendeleza nchi. Watu wa aina hii hutarajia serikali kuwafanyia hili na lile. Hawathubutu kujiuliza je, mimi nimeifanyia nini nchi yangu? Si vyema kukataa kuchangia ujenzi wa taifa na **kulaza damu** tukitarajia kuwa kila kitu kitakuwa sawa.

**Inafaa tukumbuke kwamba nchi ni kama chombo cha usafiri na kila mtu ana wajibu wake**. Kila mmoja hana budi kuhakikisha kwamba chombo hicho kimekwenda ipasavyo. Tunahitaji kuwa na bidii za mchwa za kujenga kichuguu. Tuwe na umoja wa nyuki ambao, japo ni viumbe wadogo hudiriki kutengeneza asali ambayo huwafaa wao na kuwalisha binadamu. Ikiwa vidudu hivi vinaweza kuilisha jumuiya, sembuse sisi? Wewe mwanafunzi una wajibu gani katika ujenzi wa taifa? Je, wajibu huo unautekeleza vyema au la? Kuna jambo lolote ambalo umelifanya leo linaloisaidia nchi hii? Iwapo hakuna, basi wewe ni mmoja wa wale ambao wanairudisha nchi yetu nyuma.

Mungu amemtunukia kila mmoja wetu vipawa anuwai. Ni juu yetu kuvitumia vipawa hivi kuinua uchumi wa nchi. Tukijitahidi pamoja tutaweza kutatua matatizo mengi yanayoikumba nchi. Tukumbuke kwamba kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Wananchi katika nyanja mbalimbali hawana budi kuziimarisha nyanja hizi ili kuinua hali zao za maisha. Mathalani, wakulima watumie njia za kisasa za ukulima ili kuzalisha mazao mengi. Wakifanya hivyo, tutaweza kukabiliana na baa la njaa ambalo linawadhuru wananchi wengi.

Vijana nao wana jukumu lao kwa taifa. Wewe kama mwanafunzi, unaweza kuchangia maendeleo ya nchi hii kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za shule. Ujibidiishe vilivyo, si katika masomo pekee, lakini pia katika michezo. Kwa kuiendeleza michezo ya riadha na hata ya kuigiza, utakuwa umeiendeleza nchi kwa kuukuza utamaduni wako. Isitoshe, unaweza kushiriki katika shughuli za kuzoa taka katika mtaa ulio karibu na shule yako. Ukifanya hivyo utakuwa umeitikia wito wa serikali wa kuhifadhi mazingira.

Sehemu za mashambani zinahitaji kushughulikiwa kimaendeleo. Licha ya kuwa sehemu nyingi zina rutuba, vijana wengi baada ya kupata masomo huhiari kuhamia mjini kutafuta kazi zenye hadhi. Mashamba yameachiwa wazee na bila shaka mazao yamekuwa haba.

atakayezisaidia? Je, hatujui kuwa chetu ni chetu na nguo ya kuazima haifai chochote? Ni vyema tukumbuke kuwa ikiwa tunataka kusaidiwa kuendeleza sehemu zetu, ni lazima sisi wenyewe tuwe tayari kuzitumikia kwani abebwaye hujikaza. Mapenzi kwa nchi ni muhimu mno. Shime tuungane kuijenga nchi yetu.

---

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kwamba;

A. watu wengi wana fikira zisizo za kizalendo.

B. ni kazi ya serikali pekee kuhakikisha kuwa nchi imeendelea.

C. maendeleo ya nchi yameleta mambo mengi ya kusikitisha.

D. nchi haitaendelea ikiwa wananchi wote hawatakuwa na bidii.

**32.** Kifungu kinaonyesha kuwa watu wasiokuwa na fikira za kizalendo;

A. hawathubutu kujiuliza swali lolote.

B. hutarajia serikali iwafanyie mambo kadhaa.

C. ndio wanaopasa kuendeleza nchi ya wengine.

D. hushirikiana na serikali kufanya hili na lile.

**33.** Maneno **'kulaza damu'** yana maana gani jinsi yalivyotumika katika kifungu?

A. kuwa mzembe

B. kuwa na usingizi mwingi

C. kuwa mchovu

D. kuwa na fikira mbaya

**34.** **'Inafaa tukumbuke kwamba nchi ni kama chombo cha usafiri na kila mtu ana wajibu wake.'** Kauli hii inasisitiza umuhimu wa;

A. usafiri wa majini

B. wananchi wote

C. utangamano

D. utengano

**35.** Jambo gani litakalofanyika ikiwa wananchi watakuwa na tabia kama ya nyuki?

A. Kutakuwa na asali ya kutosha kwa kila mmoja.

B. Matokeo ya kazi yetu yatatufaidi sana.

C. Uovu kama vile wizi na unyang'anyi utapungua.

D. Kazi yetu itakuwa ya faida kwetu na kwa wengine.

**36.** Ni kweli kuwa njia za kisasa za ukulima;

A. zinaweza kuongeza mazao ya kilimo iwapo zitatumika.

B. hutumiwa na wakulima wengi humu nchini ili kuzalisha mazao mengi.

C. zinaweza kuzidisha baa la njaa ambalo linawadhuru wananchi wengi.

D. zinahitaji elimu ya hali ya juu ili zilete manufaa kwetu.

**37.** Mchango wa mwanafunzi katika ujenzi wa taifa unaweza ukajitokeza vipi?

A. Kufanya bidii palipo na takataka sokoni na kushiriki kikamilifu michezoni

B. Kusoma kwa bidii, kucheza na kutunza mazingira

C. Kusafisha soko, kusoma kwa bidii na kuhifanyi mazingira

D. Kuitikia wito wa serikali, kucheza na kudumisha mazingira

**38.** Tatizo kuu la sehemu za mashambani ni lipi kulingana na kifungu?

A. Kutoa mazao ambayo ni haba.

B. Kukosa watu wa kushughulikia mashamba.

C. Kukosa rutuba ya kutosha.

D. Kukosa vijana wa kushughulikia

**39.** Kwa nini vijana wengi huhamia mijini kulingana na aya ya mwisho?

A. Kutafuta kazi

B. Kukamilisha masomo

C. Kutafuta kazi nzuri

D. Kutafuta watu wa kuwasaidia

**40.** Makala haya yanaeleza kuwa kuendelea kwa nchi yetu kunategemea;

A. kujitolea kwa kila mwananchi katika shughuli zake.

B. vijana kutohamia mijini na kuendeleza sehemu za mashambani.

C. mipango ya serikali kuimarisha maendeleo.

D. bidii ya wanafunzi masomoni ili kuimarisha elimu.

***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Ulikuwa mwendo wa saa tisa alasiri, jua lilikuwa likichoma kwa ukali. Ng'ombe waliandamana moja kwa moja hadi kwenye vivuli vya miti. Walianza kucheua na kutikisa masikio na mikia yao, dalili kuwa walifurahia nyasi hizo. Onyango na marafiki zake nao hawakuachwa nyuma. Waliwasha moto kubanika nyama ya swara waliyekuwa wamemwua. Walipata nafasi ya kupumzika kwa kuwa hawakuwa na kazi nyingi ya kuchunga ng'ombe.

Baada ya kula nyama na kushiba, waliamua kwenda **kupiga mbizi** kwenye Mto Lusumu. Waliamua kuwa ili wasijipate katika shida, wamwache mmoja wao awaangalie wanyama. Baada ya muda mfupi, wangebadilishana nafasi ili kila mmoja wao apate nafasi ya kufurahia.

Tatizo jingine lilitokea, hawakuweza kukubaliana kuhusu yule ambaye angebaki na wanyama na ni akina nani ambao wangeenda. Kila mmoja alitaka kuwa wa kwanza kujiburudisha katika maskani ya samaki. Baada ya kuwaza na kuwazua, waliamua kupiga kura. Kura ilimwangukia Sahau, kijana mcheshi lakini **msahaulifu kama ngiri.** Kijana mmoja tu ndiye aliyekuwa na saa, hivyo kijana huyo aliyeitwa Agamanya alichaguliwa kuwa mtunzawakati. Walimwahidi Sahau kuwa wangemtumia mtu baada ya dakika kumi.

Kule mtoni, mambo yalipamba moto sana. Kila mtu alijaribu alivyoweza kuonyesha ujuzi wake wa kuogelea. Mitindo mbalimbali ya kuogelea ilionyeshwa. Ninakuambia, hata samaki waliaibika. Mara Onyango alisikika akijisifu kuwa alijua kuogelea kuwashinda wote. Alizama ndani ya maji huku wengine wakipiga makofi na kushangilia. Mashindano yalinoga ungedhani kuwa mshindi angepewa kitita cha pesa. Wengine wao baada ya kutosheka, walijilaza kando ya mto na kufurahia jua kama mijusi. Hakika, walifurahia na kuona raha bin starehe.

"Salaale! Oneni wasichana wanakuja kuchota maji. Mtapatwa mkiwa mmevaa suti ya Mungu!" Waligutuka na kushangaa nusura wazimie. Aliyekuwa akiwaambia hivyo hakuwa mwingine ila Sahau. Lililowatia wasiwasi zaidi ni kuwa yeye ndiye aliyeachiwa kazi ya kuwatunza ng'ombe.

"Jameni! Ulikujaje huku?" Walimwuliza.

Lililowashangaza hata mno ni kuwa Sahau alikuwa ameogelea na wao kwa zaidi ya saa nzima. Alikuwa amejiunga na wao bila wao kujua. Mambo yaliwaharibikia walipokosa kuziona nguo zao. Damu iliwasisimka mwilini. Ng'ombe je! Hawakuonekana kokote.

Vijana hao sita walichanganyikiwa ungedhani kuwa ni mtu aliyepotea njia wakati wa usiku. Hawakujua la kufanya, waliangaliana tu ungedhani kuwa hiyo ndiyo iliyokuwa mara yao ya kwanza kuonana. Kilichowazindua ni sauti ya radi ya chifu. Aliandamana na wazazi wao huku wakiwa wamezibeba nguo za vijana watano kati yao. Sahau pekee ndiye aliyekuwa na nguo zake.

Hapo **walitambua kilichomtoa kanga manyoya.** Walitambua kwa nini wazazi wao

kutembea na marafiki zake waliokuwa na tabia mbaya. Kijana huyo ambaye kitambo alikuwa mtiifu sana alikuwa amebadilika sana baada kuanza kutembea na vijana hao wengine. Kuanzia siku hiyo, Onyango aliamua kuwa angefuata ushauri na kujiepusha na vijana wale waliopotoka.

---

**41.** Jambo gani hasa lililowapeleka ng'ombe kwenye vivuli vya miti?
A. Walikuwa wameshiba
B. Walisumbuliwa na ukali wa jua
C. Walitafuta mahali pa kucheua vizuri
D. Walikuwa wamechoka kusimama

**42.** Nahau '**kupiga mbizi**' ina maana gani?
A. kufurahia
B. kuogelea
C. kucheza majini
D. kuvua samaki

**43.** Ahadi ya kubadilishana nafasi kila baada ya dakika kumi haikutekelezwa, kosa hili lilisababishwa na nani hasa?
A. Agamanya
B. Onyango
C. Sahau
D. Sahau na Onyango

**44.** Maneno '**msahaulifu kama ngiri**' yametumia fani gani ya lugha?
A. tashbihi
B. istiara
C. tashihisi
D. tanakali

**45.** Vijana wangapi waliofaa kuogelea kwa wakati mmoja?
A. mmoja
B. sita
C. watano
D. wanne

**46.** Yawezekana kuwa kwa nini vijana hao hawakumwona Sahau alipojiunga nao?
A. Walikuwa wameangalia upande mwingine.
B. Walikuwa wamezama ndani ya maji.
C. Mawazo yao yalikuwa yamepotelea katika kuogelea.
D. Sahau alijifichaficha hadi alipofika walipokuwa.

**47.** Kubadilika kwa tabia za Onyango na kuwa mwenye tabia mbaya kunaweza kuelezwa kwa methali gani?
A. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.
B. Majuto ni mjukuu huja kinyume.
C. Damu ni nzito kuliko maji.
D. Nazi mbovu harabu ya nzima.

**48.** Katika aya ya tano, hofu kuu ya vijana hao ilitokana na;
A. kupotea kwa nguo zao.
B. kupatikana na chifu na wazazi wao.
C. kutojua kule ng'ombe walikokuwa.
D. kupatwa na wasichana wakiwa uchi.

**49.** Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa vijana hao '**walitambua kilichomtoa kanga manyoya**'?
A. waliadhibiwa
B. hawakurudishiwa nguo
C. walifukuzwa nyumbani
D. walichapwa

**50.** Kosa kuu la vijana hao lilikuwa lipi?
A. Kwenda kuogelea badala ya kuwachunga ng'ombe.
B. Kumwachia Sahau ng'ombe badala ya kwenda naye kuogelea.
C. Kuogelea bila kumwacha mtu wa kuchunga nguo zao.
D. Kutopeleka mtu wa kuwaangalia ng'ombe ili Sahau naye aogelee.